Somo la 17

MAUMBILE NA KAZI YA YESU KRISTO

"Kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo" - Waebrania 2:14.

KUNA mitazamo mikali aina mbili kumhusu Yesu katika ulimwengu wa Ukristo wa jadi. Moja inamlinganisha Yesu na Baba katika maeneo yote ya toka milele. Nyingine inasema alikuwa mtu tu wa kawaida, yaani mtu mzuri na mfano mzuri wa kimungu. Ukweli wa Maandiko yako katikati ya pande hizi mbili zilizo na misimamo mikali.

Dhana ya jadi ya "Utatu", kuweka Yesu kwenye usawa mmoja wa milele na Mungu, ni kinyume na mwelekeo mzima wa Maandiko. Hii inatolewa mfano kwa dondoo zifuatazo, zinazoonyesha Mwana ni tofauti kabisa, na anamtegemea Baba -

"Mimi (Yesu) siwezi kwa uwezo wangu mwenyewe kufanya kitu kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo na hukumu yangu ni haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka"(Yohana 5:30)

Kama Yesu (kwa mujibu wa nadharia ya Utatu) ni sehemu muhimu ya" Mungu Mmoja " hakuna uwezekano wa kuwepo kwa matakwa mawili mbalimbali - mapenzi yake na yale ya Baba. Maandiko yako wazi sana kuwa kulikuwa na matakwa au mapenzi mawili tofauti:

"Na, akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba, akisema: Baba yangu, kama inawezekana, acha kikombe hiki cha mateso kinipite; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe." (Mathayo 26: 39)

"Mafunzo yangu si yangu, bali ni yake yeye aliyenituma" (Yohana 7:16).

"Na uzima wa milele ni huu, wakujue wewe, Mungu wa kweli, na Yesu Kristo, uliyemtuma" (Yohana 17: 3).

"... Kuna Mungu mmoja tu, Baba…. na Bwana mmoja Yesu Kristo" (1 Wakorintho 8: 6).

"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu" (1 Timotheo 2: 5).

Kumbuka kuwa nukuu hii ya mwisho, hasa kubainisha Yesu na "Mungu Mmoja" inayomwita yeye "binadamu" iliandikwa muda mrefu baada ya Yesu kufufuka na kutukuzwa.

Biblia inafundisha wazi kwamba - Baba ni wa milele na asiyejulikana. Mwanawe ni dhihirisho la Baba katika binadamu aliyezaliwa na operesheni ya Roho juu ya Mariamu, mtoto mchanga alizaliwa na kukua na kuendelea kujifunza kama watu wote wengine.

Roho Takatifu ni mkusanyiko wa nguvu ya Mungu, kuna "Roho huria ambayo hujaza mbingu na nchi." Takatifu kwa ufupi inamaanisha kutengwa kwa ajili ya matumizi maalum ya kimungu. Mungu ni mkuu juu ya yote, hata juu ya Kristo - "Kichwa cha Kristo ni Mungu" (1 Wakorintho 11: 3).

"Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye aliyemtiishia vitu vyote, ili kwamba Mungu awe YOTE KATIKA WOTE." (1 Wakorintho 15:28).

Mwanadamu Kristo Yesu chini ya Mungu, ili Mungu awe juu ya yote: kwamba hii ni taswira ya mwisho iliyotolewa katika Maandiko.

Kwa mara nyingine, Mungu alisema anajua mambo yote - "Asema Bwana, ajulishaye hayo tangu milele." (Matendo 15:18).

Tofauti na Yesu, na ni katika siku za mwili wake unaokufa alifundisha kuwa angeweza kurudi siku moja duniani kwa heshima, lakini kwa uwazi. Inasema kwamba hakuna MTU, hata yeye mwenyewe, anayejua wakati wa kurudi kwake, na kwamba wakati huo unajulikana na Mungu Mmoja wa kweli pekee - "Walakini habari ya siku na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, WALA MWANA, ila Baba" (Marko 13:32).

Hili ni pigo baya kwa wale ambao wanaounga mkono nadharia ya Utatu. Wao hujaribu kukwepa uzito wake kwa kubuni Kristo aina mbili tofauti, mmoja ambaye ni Mungu, na Mwenye kujua vitu vyote, na wakati huo huo hajui baadhi ya mambo ambayo mwingine anafanya! Huu ni upuzi ambao Maandiko hauyajui kabisa na inabaki na unyofu wake. .

Nadharia ya "Waunitaria" - maana nyingine tofauti na nadharia ya "Utatu" - ni kwamba Yusufu alikuwa baba halisi wa Yesu. Lakini Mungu alionyesha Yusufu mwenyewe, ya kuwa (Yusufu) hakuwa baba wa Yesu. Yusufu alikuwa na nia ya kumweka Mariamu kando, mchumba na mke mtarajiwa, wakati "alipatikana na mtoto", lakini akaongozwa na malaika –

"Yusufu, Ee mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu awe mke wako, maana amekuwa mja mzito kwa uwezo wa Roho Takatifu (Mathayo 1:20)

Mariamu hapo awali alikuwa ameonyeshwa kuwa Mungu angekuwa Baba wa Yesu- "Roho Takatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa takatifu, Mwana wa Mungu "(Luka 1:35).

Waunitaria wana msimamo finyu juu ya jambo hili kuliko wale wa Utatu. Wakati Utatu unapuuza vifungu, au unajaribu kueleza kivingine, Waunitaria hukataa kabisa ukweli wa vifungu vyovyote vilivyo na mgogoro na nadharia zao. Kwa sababu ya mtazamo wa sasa usio wa imani wa makanisa kwa Biblia kama Neno lililo na pumzi ya Mungu, njia hii ya kubadili maneno na kuandika upya maandiko inaongezeka.

Ukweli upo katika uwiano kati ya hitilafu baina ya waumini wa Utatu na Waunitaria. Ukweli ni kwamba Kristo alikuwa ni mtu maalum, aliyezaliwa kupitia kwa Mariamu kutoka kwa Mungu kwa njia ya Roho Takatifu; hasa kupewa nguvu na Mungu kwa ajili ya kusudi maalum - mtu ambaye Mungu alikaa ndani yake na kujidhihirisha kwa wanadamu - mtu mkamilifu ambaye alitii kikamilifu, na alishinda "mwenendo wa dhambi" kwa ukamilifu, "Dhambi katika mwili", "ibilisi aliye na nguvu ya kifo ". Hii ilikuwa ni kazi ambayo hakuna mtu wa kawaida, asiyesaidiwa, mwenye nguvu za kimwili aliyezaliwa na binadamu anaweza kukamilisha. Maisha kamilifu na kifo cha Kristo kama sadaka ilikuwa kazi ya Mungu kupitia kwake - ambayo aliikubali kikamilifu hata hicho kifo cha kutisha, kwa kujitoa kwa mapenzi yake mwenyewe, kwa hiari yake, pasi na kuruhusu mwili kuingilia azimio lake. Kusudi la Mungu lililotangazwa ni kuwa Yesu alikuja duniani ili aondoe dhambi:

KUMBUKA "Dhambi katika mwili"

"Dhambi-katika-mwili-" ni istilahi ngumu kwa wengi kuielewa, kwa kuwa wanahisi kwamba kwa namna fulani ni kusema kwamba kuna tendo halisi la kukosa katika mwili, au kwamba kumiliki tu kwa dhambi katika mwili ni hali ya kukosa. Sivyo, fungu hili linarejelea matumizi bayana ya neno dhambi, na kwa matumizi ya tamathali ya semi iitwayo ‘metenomi”. Labda mfano bora wa namna ya kuelewa haswa istilahi hii ni kuangalia kurasa za Biblia zenyewe, kama katika 2 Wafalme 4:40. "... na ikawa, walipokuwa wakila chakula, (watoto wa manabii) wakapiga kelele, na kusema, mauti imo sufuriani Ee mtu wa Mungu.Wala hawakuweza kula. "Sasa, hii haikumaanisha kuwa kulikuwa na wafu halisi katika sufuria. Ina maana tu kwamba kulikuwa na kitu katika sufuria ambacho bila shaka kingefanya mtu aliye hai kuwa maiti. "Kifo" kilimaainisha kwa uhalisia "kwamba kile ambacho husababisha kifo". Kanuni hiyo ya utafsiri inatumika kwa msemo kwamba kuna "dhambi katika mwili". Haimaanishi kwamba mwili una vitendo halisi vya hali ya kukosa. "Dhambi", katika wazo hilo inamaanisha kwamba maana yake halisi ni "yale yanayoweza kusababisha dhambi". Inamaanisha kwamba kuna yaliyomo katika maumbile ya asili yetu ambayo hatuwezi kuyaepuka na husababisha kila mmoja wetu kufanya vitendo vya uvunjaji sheria (asiyejumuishwa kwa sheria hii ni Kristo, ambaye bila jasho na kila mara aliepuka ushawishi huo mara kwa mara kwa kutumia Maandiko kwa upendo wa kumtii Baba na kufanya mapenzi yake maishani mwake).

"Dhambi katika mwili" ni sawa na istilahi zingine katika Maandiko kama vile "mwenendo wa dhambi", "sheria ya dhambi ndani ya viungo vyangu", "ibilisi", "mtu wa kale", "mwili", "mwili wa dhambi ", nk "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu "(Yohana 1:29). Na hii ilikamilika kwa jinsi gani? - "Yeye aondoaye dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake" (Waebrania 9:26.).

Hapa kuna dhana ya kiroho muhimu na yenye maana na madhumuni na ufanisi wa kifo chake - ALIONDOA DHAMBI kwa kujitoa kama dhabihu mwenyewe. Wakati wa maisha yake yote Kwa ukamilifu kabisa alipinga, akashinda, akaangusha, akaangamiza, alizuia “dhambi katika

mwili” "Dhambi-katika-mwili," "mwenendo wa dhambi," "sheria ya dhambi pamoja na uzao wote wa Adamu yeye akiwa mmoja wao, akawa mwakilishi wa kweli - Mkamilifu, Mtu Bora.

Na kisha, katika kifo chake cha hiari, kwa upendo wake akajiwasilisha kwa mapenzi ya Baba, akapigilia misumari mwili ule najisi wa dhambi, mwili uliolaaniwa wa dhambi, huo "Mwili wa Dhambi", kwenye mti - kwa kuhukumu na kufutilia mbali mwili wa dhambi, na kwa kuonyesha utukufu wa haki ya Mungu yaliyohitaji utakatifu kwa kusulubisha ule mwili kama njia ya pekee yenye maadili na mlango mwembamba ---kupitia kwa mauti iliyowafikia watu wenye dhambi--- ili wafikie uzima wa milele, usio na dhambi wala mauti.

Mwanzo kwake yeye, mwenyewe, na kwanza kibnafsi (lakini kwa sababu ya ndugu zake) - kwa kutoa utakaso wa sadaka ya kiroho unaohitajika kwa wanadamu - aliuvunja mnato wa dhambi juu ya watu, akavunja milango ya mauti, na akafufuka kwa ushindi na uzima wa milele usiokuwa na dhambi - tena usiotawaliwa na hisia za mwili wa dhambi.

Na, kwa rehema na upendo wa Mungu, wote ambao hujikana na kuwa pamoja kabisa na yeye, na kuwa waaminifu hadi kufa, wanashiriki ushindi wake, sadaka yake - ilinunua ukombozi wake na utakaso, ufufuo wake, na maisha yake ya utukufu wa milele.

Ufafanuzi ulio Ufunguo wa Biblia - "kana/kataa" maana yake ni kukataa kukubali kama halali au ni ukweli, kwa kutokuwa na ushirika wowote. Na "sadaka" na "iliyotolewa dhabihu" maana kama neno la Kiswahili kwa ufupi linamaanisha "kazi takatifu." Hata hivyo, katika Biblia ya Kiebrania na Kigiriki ina maana mbili.

1. Kusababisha kupaa, kumtolea Mungu, kuleta karibu na Mungu.

2. Kuchinja, kuua.

Yesu alisema: "Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo." (Yohana 10:15).

Paulo aliandika: "Yesu Kristo amekomesha nguvu za kifo, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili" (2 Timotheo 1:10).

Na Petro: "Hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

Kwa kweli, hakuna kabisa uwezekano wa maisha nje ya Kristo - "Yeye aliye naye Mwana wa Mungu anao huo uzima, asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima" (1 Yohana 5:12). "Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu ... HAMNA UZIMA ndani yenu" (Yohana 6:53).

"Mtu haji kwa Baba, ila kwa NJIA YA MIMI" (Yohana 14: 6).

Wokovu unaunganishwa moja kwa moja na mwanzo wa kuonekana kwa Yesu. Na huu sio tu "mfano wa maadili" ambao Yesu aliuwekea watu wote kuufuata, lakini kwa misingi ya mara

moja-kwa-wote mfano wa vitendo na mafanikio yake kuhusiana na dhambi na asili ya dhambi -- "Dhambi katika mwili" - "sheria ya Dhambi katika mwili" - kwa kipindi cha maisha na kifo chake, kufuatia baadaye ufufuo na kutukuzwa kwake. Matumizi halisi ya neno "Mwana" kama ilivyotumika kwa Yesu - mara kwa mara na kwa msisitizo - inaonyesha kwamba kuwepo kwake kulipatikana kutoka mahali fulani, na kwamba yeye hakuwapo tangu hapo. Maelezo "Mwana wa Mungu" inaonyesha chanzo cha maisha yake na kuwepo kwake. Mungu alitangaza kwake kiunabii - "Ndiwe Mwanangu, Mimi leo nimekuzaa" (Zaburi 2: 7).

Hapa ni mwanzo maalum. Ingawa Yesu sasa ana asili, maisha yasiyokuwa na mwisho, ambayo amepewa na Mungu:

"Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo ALIMPA NA MWANA kuwa na uzima nafsini mwake" (Yohana 5:26).

Ilikuwa IMEPEANWA kwake - hivyo ni wazi kulikuwa na wakati ambapo yeye hakuwa nayo. Yesu hakuzaliwa kwa nguvu za kimwili, lakini moja kwa moja kwa mapenzi na uendeleshaji wa Mungu.

Mariamu alimzaa Yesu kupitia kwa njia ya Roho Takatifu. Hivi ndivyo alivyokuwa "Mwana wa Mungu", kama tunavyosoma katika Luka 1: 35-

"Roho Takatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu"

Ingawa alikuwa Mwana wa Mungu kwa kuzaliwa kwa njia ya kipekee, alikuwa ni mwili na damu ya uzao wa Adamu. "Kwa kuwa, basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo. Yeye hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote"(Waebrania. 2:14 17).

"Yeye asiyejua dhambi (alimfanya kuwa dhambi) kwa ajili yetu, " (2 Wakorintho 5:21).

Katika tabia na vitendo alikuwa hana dhambi kabisa: kwa hiyo hii inaweza tu kutumika kwa mwili wake wa kufa, maumbile yaliyolaaniwa kwa dhambi, ambayo kutokana na Mariamu ilikuwa ni mwili ulio wa dhambi wa Adamu. Kwa hivyo Paulo alisema hivi kuhusu Yesu - "Mungu alimtuma Mwana wake katika mfano wa mwili ulio wa dhambi" (Warumi 8: 3).

"Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke" (Wagalatia 4: 4).

"Katika uzao wa Daudi kwa jinsi ya mwili" (Warumi 1: 3).

Kazi na shughuli kubwa ya Kristo ilikuwa kumwokoa mwanadamu kutokana na dhambi kwa kushinda maumbile ya dhambi kikamilifu: maisha ya utakatifu, maisha ya kujitolea yaliyofikia upeo wa kifo kama dhabihu ya kuondoa na kusafisha maumbile aliyochukua kwa kushiriki asili ya wanadamu wote, na ambayo ilimfanya awe mmoja na sisi sote. Hii ni kazi nzuri ya Mungu

ambapo Kristo, kama mmoja wetu - Mwakilishi wetu na mfano- anafikia ushindi mwenyewe dhidi ya jamii nzima, na utakaso kutoka, kwa dhambi: ili tuweze – kuondolewa kabisa "nafsi", na kujiunga kabisa naye – tuweze, kwa hekima ya Mungu, kupata rehema na upendo, na kuwa na sehemu katika uzima wa milele kupitia kwa ushindi wa Yesu juu ya dhambi.

Tukipoteza dhana hii, tutakuwa tumepoteza ufunguo wa msingi katika kuelewa ujumbe na kusudi la Mungu. Yesu mara kwa mara anatajwa kama "mwanadamu" –

"Mtu aliyedhihirishwa na Mungu ... na miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya, kwa mkono wake" (Matendo 2:22).

"Mwanadamu Kristo Yesu" (1 Timotheo 2: 5) hapo ametofautishwa na 'Mungu mmoja': "Mungu atauhukumu ulimwengu kwa haki kwa njia ya mtu aliyemteua" (Matendo 17:30).

Kumbuka kuwa kauli hizi zote anapoitwa "mtu" yalifanywa baada ya kufufuka kwake, utukufu na kupaa mbinguni. Yeye daima huitwa mtu - hata katika hali yake ya sasa na msimamo

-- KAMWE haitwi Mungu: ingawa, kama tukizingatia katika Somo la 16, katika kuwajibu Wayahudi ambao walimpinga kwa kujiita "Mwana wa Mungu" aliwambia kuwa wale WOTE ambao wana uhusiano na Mungu na ambao kwa namna yoyote ile humwakilisha wanapewa jina "mungu" (Waebrania: elohim, Wenye Nguvu) kwa maana inayotokana - "Je, haikuandikwa kwa sheria yenu, `mimi (Mungu) nimesema, ninyi ni miungu? Kama Aliwaita 'miungu' nao kupitia kwao ndio neno la Mungu lilikuja…" (Yohana 10:34 35).

Na ameahidi kuwapa Jina la Mungu wote walio waaminifu –

"Yeye ashindaye… nitaandika juu yake jina la Mungu wangu..." (Ufunuo 3:12).

Lakini hii ni tofauti kabisa na kusema kwamba Yesu ni mmoja wa watatu walio wa milele na wenye nguvu sawa katika sehemu tatu inayoitwa "Utatu;" ni lazima kujiepusha nayo. Yesu alihukumiwa na kuadibishwa kama Adamu, akafanikiwa ambapo Adamu alishindwa - "Na ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata" (Waebrania 5: 8.). Fikiria haya kwa muda mrefu na kwa uketo - ALIJIFUNZA kutii kupitia kwa mateso. Inaoana vizuri na picha ya kweli ya Biblia, Utatu ni mtazamo wa upuzi. Yesu alikuwa dhihirisho la Mungu kwa nguvu ya Roho Takatifu, lakini hakuwa Mungu mwenyewe. Roho Takatifu ilishuka kutoka kwa Mungu juu ya Yesu katika sura ya mwili wa hua wakati Yohana alimbatiza huko Yordani. Hivyo tunasoma katika (Matendo 10:38) - "Mungu alivyomtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Takatifu na nguvu."

Kwa mara nyingine, nukuu hii inaonyesha ... ***

1) Kwamba Mungu ni mkuu kuliko Yesu: Yeye ndiye Mwamuzi na Mpaji; Yesu ni mpokeaji na mtiifu;

2) Kwamba Yesu anamtegemea Baba, na si sehemu ya nguvu sawa ya "Utatu"; na

3) Kwamba Roho Takatifu sio mtu na sio sawa na Mungu, bali ni nguvu za Mungu anazozitumia kuweza kuwatia mafuta wengine katika vipimo na viwango mbalimbali (tazama Yohana 3:34).

Yesu hakufanya miujiza kabla ya kutiwa mafuta kwa nguvu ya Roho. Yeye hakuwa na nguvu yake mwenyewe. Alisema -

"Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe" (Yohana 5:30).

"Baba yu ndani yangu huzifanya kazi zake" (Yohana 14:10).

Na usemi wake wa unyonge akiwa kwenye mti, akiwa hoi -

"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mathayo 27:46).

Kwa mara nyingine tena, nadharia ya Utatu inakumbana na hali ya kutisha na isiyoeleweka: lakini tuna maelezo wazi, rahisi, na kipengele kizuri cha ukweli wa Mungu. Mungu alitoa Roho Takatifu, na, kama inavyofaa lengo lake Mungu, Mungu aliondoa Roho Takatifu kutoka kwa Yesu.

Yesu alikuwa "mwili uliotayarishwa" kwa ajili ya kutiwa mafuta na Mungu, na kwa ajili ya kazi ya wokovu iliyotabiriwa kwa kushinda, kuharibu na kumsulubisha Ibilisi hadharani, "Dhambi katika mwili" (Waebrania 10: 5-7) –

"Dhabihu na toleo hungetaka, lakini mwili uliniwekea mimi tayari. Sadaka za kuteketezwa au za kuondoa dhambi hazijakupendeza. Ndipo nikasema: `Niko hapa (katika kiasi la kitabu kilichoandikiwa) kufanya mapenzi yako, Mungu:

Huyu ni "mwanadamu Kristo Yesu "akimzungumzia Mungu mmoja wa milele asiyeumbwa aliyemuumba yeye, na kwa kumtii yeye aliyakataa mapenzi yake mwenyewe, na kwa upendo akanyenyekea kiasi cha kufanya mapenzi ya Baba.

Asili yake mwenyewe ya kibinadamu haikuwa ya kuteseka na kufa juu ya mti –

"Aba, Baba, Yote yawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe" (Marko 14 : 36).

"Sasa roho yangu imefadhaika; nami nisemeje? Baba, uniokoe katika saa hii? Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii. Baba, ulitukuze jina lako!" (Yohana 12: 27-28).

Baada ya Yesu kutiwa mafuta, alikuwa dhihirisho kamili la Mungu katika mwili --

Lakini VYOTE pia vyatokana na Mungu… Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." (2 Wakorintho 5: 18-19)

Wakati Yesu alipokwisha kutukuzwa, asili yake ya mwanadamu ilibadilika na kuwa yenye asili ya Roho: asili ya nyama na damu iligeuka na kuwa asili ya kutokufa. Hivyo ndivyo alivyo sasa –

"Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu (uungu, asili ya kiroho) kwa jinsi ya kimwili" (Wakolosai 2: 9)

Lakini yeye hajaacha kujitambulisha na ndugu na dada zake, hajasahau kumbukumbu yake na hisia ya majaribio ya kujifunza na kushinda. Yeye bado ni MTU -- ingawa sasa ametukuzwa, ni mtu aliye na uzima wa milele - kama ndugu zake wote wanavyotumainia –

"Kwa kuwa hakuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu." (Waebrania 4:15)

Basi, tunaweza kumkaribia Mungu kwa njia ya kuhani wetu wa upatanisho ambaye anajua udhaifu wetu:

"Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa" (Waebrania 2:18).

Tunajua, kwa hakika, kwamba Mungu hawezi kujaribiwa –

"Mtu ajaribiwapo,asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu yeyote:" (Yakobo 1:13).

Kwa hiyo, kwa nguvu tu ya mstari huo mmoja, Yesu sio Mungu.

Wakati wa siku za ujio wake wa kwanza, kama ushahidi katika kumbukumbu ya Injili, yeye siku zote alifanya mambo ambayo yalimradhi Baba yake. Yeye daima na kwa wazi alidhihirisha tabia ya Baba kwa utakatifu na ukamilifu. Alikuwa Immanueli, "Mungu pamoja nasi", yaani –

"Mungu kudhihirishwa katika mwili" (1 Timotheo 3:16).

Kwa hiyo angesema na Filipo –

"Aliyeniona mimi amemwona Baba" (Yohana 14: 9).

Paulo alisema:

"Kristo ni mfano wa Mungu asiyeonekana" (Wakolosai 1:15).

"Yeye ni mng'ao wa utukufu wa Mungu, na chapa ya nafsi yake" (Waebrania 1: 3.). ***

Wale ambao waliona Yesu aliyepakwa mafuta waliona uwakilishi kamili wa Mungu, wazi kwa macho ya binadamu. Na Kristo ni mfano halisi wa kusudi la Mungu, onyesho katika watu wa Roho wa Mungu na Nguvu-

"Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli "(Yohana 1:14).

"Mungu hakutoa kwake Roho kwa kipimo" (Yohana 3:24).

"Katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu (uungu) kwa jinsi ya kimwili" (Wakolosai 2: 9)

Ukweli wa msingi kuhusu Yesu Kristo ni huu. Yeye –

- Alikuwa mtu, wa ukoo ya Adamu, kazaliwa kupitia kwa Mariamu na Roho Takatifu, mtoto mchanga mnyonge, alizaliwa Bethlehemu.
- Kukua mtu mzima, na kuongezeka katika hekima, kujifunza utiifu.
- Aliendelea kuwa mtu kibinafsi, seremala, mpaka alipopakwa mafuta kwa Roho na Mungu wakati wa ubatizo wake na Yohana Mbatizaji.
- Aliuawa katika udhaifu, baada ya kufanya mambo yaliyomo katika Injili (matendo ya Mungu ndani yake, akiupatanisha ulimwengu).
- Aliondolewa nguvu za Mungu wakati alipokuwa kwenye mti. – Alifufuliwa > kutoka kwa wafu na Baba, na sasa yuko hai hata milele, mtu ambaye ametukuzwa na ana uzima wa milele, kama ndugu zake walivyo na matumaini ya kuwa nayo.

Haya ni mafundisho thabiti ya Maandiko kuhusu Yesu. Vifungu kama vile. . .

"Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko" (Yohana 8:58). . . inakubaliana vema na ufunuo uliotolewa kwa ujumla. Yesu alikuwa kiini katika madhumuni ya Mungu. Alikuwa "kabla Ibrahimu" katika mpango. Zaidi ya hayo, Mungu alisema kupitia kwake; yeye alitangaza neno la Mungu kama dhihirisho la Mungu na kinywa chake, kama alivyosema. Mungu, ambaye alikuwa ndani yake yeye na alizungumza kupitia kwake, alikuwa Yehova wa milele: "Mimi ni," au kwa usahihi zaidi, "Mimi nitakaye kuwa."

Ibrahimu, kutambua umuhimu wa taifa, na kwamba Mungu "atamtoa kondoo" kutupilia mbali dhambi ya ulimwengu (Mwanzo 22: 8), aliweza kutazamia ujio wa Yesu, na "ilikuwa furaha" katika kuona siku ya Kristo (Yohana 8:56).

Ufafanuzi wa Kipengele cha Biblia

"Chini ya" - sekondari, kidogo, duni

"Kristo kwa wingi" - neno linalotumiwa kuonyesha umati wa wale waliokombolewa kupitia kwa Kristo na wanasimama pamoja naye baada ya ufufuo na hukumu

Hii ni hisia ambapo Yesu alikuwa na "utukufu kwa Baba kabla ya ulimwengu kuwako" (Yohana 15: 7); kama, katika maana ya chini, mwili wake, waliokombolewa, Kristo kwa wingi, walikuwa na "utukufu" sawia na Mungu "tangu milele kabla ya dunia kuanza" - "Mungu ALITUCHAGUA

katika Kristo kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu ... alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe "(Waefeso 1: 4 5).

"Neema hiyo tulipewa katika Kristo tangu milele" (2 Timotheo 1: 9).

Vile vile, Mungu alimwambia Yeremia: "Kabla sijakuumba katika tumbo, NILIKUJUA wewe ni nani ... na nikakutakasa " (1: 5).

Na alimwita Koreshi kwa jina, kana kwamba alikuwepo, zaidi ya miaka 100 kabla ya kuzaliwa kwake (na kupelekea wachambuzi waliokataliwa na kuchanganyikiwa kugawa kitabu cha Isaya katika sehemu mbili) - "Bwana asema hivi kwa masihi wake, kwa Koreshi, ambaye nimemshika mkono wake wa kuume "(Isaya 45: 1).

Kweli alisema, na ni utukufu wa kweli: "Mimi na Baba tu umoja" (Yohana 10:30).

Kristo na Baba walikuwa daima katika umoja kamilifu na utulivu. Yeye hangekuwa ni "Dhihirisho la Mungu kati ya wanadamu" kama hawangekuwa hivyo; wala hangekuwa sadaka kamili inayohitajika kwa ajili ya utakaso wa wanadamu kutoka kwa dhambi katika malengo yake yote na masuala.

Yeye ni hata zaidi sasa "mmoja na Mungu" kuliko wakati alitoa taarifa hiyo, kwa sasa yeye ni mmoja na Yeye katika mwili wa Uungu.

Umoja na Mungu ni lengo na tuzo linalowekwa mbele ya wote. Yeye mwenyewe aliomba kuhusu ndugu na dada wake katika vizazi vyote ulimwenguni –

"Wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu" (Yohana 17:21).

Yesu hakuwepo kabla ya kuzaliwa kwake halisi kupitia kwa Mariamu. Ni lazima kuukubali ukweli huu ulio wazi, wenye uhalisia, uliorekodiwa kuhusu kuzaliwa kwake na kukua kufikia ujuzi. Lakini alikuwa, kutoka mwanzo, aliyeteuliwa kimbele awe njia ya wokovu kwa kutolewa na Mungu, kama ilivyodhihirishwa wazi katika bustani ya Edeni, na kwa njia ya Maandiko yote. Misemo yake yenye uzito na ishara, iliyo na msingi yake juu ya nafasi yake katika Madhumuni ya kiroho, na makao ya Mungu ndani yake na anavyozungumza kupitia kwake, lazima ieleweke kwa misingi ya kutotilia shaka, mambo halisi, UKWELI uliofunuliwa juu ya kuzaliwa kwake kama mtoto mchanga, kukua kwa hatua hadi akawa mtu mzima, "kuongezeka kwa hekima," "kujifunza utiifu," kuwa "na ukamilifu," kushinda ", nk (Luka 2:52; Waebrania 5: 8 9; 2:10; Yohana 16: 33).

Na atarudi duniani katika ujio wa pili, unaokuja hivi karibuni, wakati atakapodhibiti mataifa yote kwa haki na mapenzi ya Baba yake. Na wakati kazi itakapokamilika kabisa, mwisho wa Milenia, atajiwasilisha mwenyewe kwa Baba ili Mungu awe "YOTE KATIKA YOTE" –

"Wakati mambo yote yatadhibitiwa chini ya Utawala wake (Kristo), basi mwana mwenyewe atakuwa chini yake, aliyeweka vitu vyote chini yake, ili Mungu awe YOTE KWA YOTE. "(1 Wakorintho 15:28

MASWALI YA SOMO LA 17

1. Ni nadharia zipi mbili zisizo za kimaandiko ya kawaida yanayoshikiliwa kuhusu nafasi ya Yesu kuhusiana na Mungu?

2. Je, ingewezekana Yesu mwenyewe kufanya kazi ya miujiza bila nguvu za Mungu?

3. Nani alikuwa Baba wa Yesu?

4. Je, Yesu alizaliwa na maarifa ya yote, kama vile angekuwa nayo kama angekuwa ni sehemu ya milele, nguvu sawa, Mwenye ujuzi wote wa ‘Utatu’?

5. Vifungu gani vya maandiko matakatifu vinaonyesha kuwa Yusufu hakuwa Baba wa Yesu?

6. Mungu alikuwa na kusudi gani katika kumleta Yesu katika ulimwengu?

7. Ni kwa njia gani ambapo kifo cha mtu mwenye haki na mtiifu kilidhihirisha haki na wema wa Mola, na kumtukuza Mungu?

8. Ni nini kilifaa kuangamizwa kwa kutolewa sadaka kwa umma kwa kuuawa kabla Kristo hajaupata uzima wa milele na kuwa Safina ya usalama kwa watu wake kukimbilia?

9. Je, tunashiriki kivipi utakaso na ukombozi wa Kristo alioukamilisha kwa nafsi yake mwenyewe?

10. Je, wokovu unapatikana tu kwa kufuata maadili mema ya maisha ya Yesu, bila kifo chake kama dhabihu na ufufuo wake? (Toa vifungu)

11. Je, maelezo 'Mwana wa Mungu' yanafundisha nini kuhusu kuwapo kwa Yesu?

12. Yesu alikuwa na mwili uliochafuliwa na dhambi na ulio na asili ya damu kama sisi?

13. Je, Yesu alikuwa wa ukoo wa Daudi, Ibrahimu na Adamu?

14. Je, Yesu alikuwa binadamu? (Toa vifungu).

15. Je, bado yeye ni mtu, mwanadamu?

16. Je, Yesu ‘alijifunza’ vipi ‘kutii’?

17. Alifanywa ‘mkamilifu’ kwa njia gani?

18. Yesu alipata lini na kutoa kwa nani uwezo wa kufanya miujiza?

19. Yesu aliweza kupata Roho Takatifu kivipi?

20. Ni kwa jinsi gani Yesu angesema, 'Mtu yeyote anionapo mimi amemwona Baba'?

21. Ni kwa njia gani Yesu alikuwa kabla ya Ibrahimu?

22. Je, alikuwaje ‘mmoja na Baba’?

23. Kwa sababu gani huwaombea ndugu zake kuhusu hili?

24. Yesu atachukua nafasi gani Mungu akiwepo baada ya Milenia?

s